**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

# SCHOOL BASED ASSESSMENT

## KISWAHILI SEHEMU A

## Gredi ya 7

**NAKALA YA MWANAFUNZI**

**SEPTEMBA 2024**

**© KNEC 2024** **GEUZA UKURASA**

Je, umewahi kuwaza kuhusu jinsi ambavyo jamii ingekuwa iwapo kila mtu angekosa maadili ya kibinafsi? Fikiria kwa mfano, unataka kuingia darasani, naye mwenzako amesimama mlangoni, hataki kukupisha. Utahisi vipi? Bila shaka utaudhika. Utamwambia, “Simile!” Hapo utakuwa umemwomba akupe nafasi upite. Huenda hata ukatumia mfano wa huyo mwenzako kuwafunza wengine kuhusu umuhimu wa maadili ya mtu binfasi. Utawaambia kwamba mtu huanza kujifunza maadili akiwa mchanga. Lau sivyo itakuwa vigumu kuyapata. Bila shaka unafahamu kwamba samaki hukunjwa angali mbichi.

Yakini, maadili ya mtu binafsi ni nguzo kuu katika kujenga mshikamano wa kijamii. Matendo madogomadogo ya kimaadili kama vile kuamkua wengine, kushukuru kwa mema, kuyaheshimu maoni ya wengine, na kuwahi shughuli muhimu, hupalilia mahusiano mema.